

*Kikoi*

**Swahili transcript:**

Vazi jingine ambalo ningependa kulizungumzia kwambawatanzania pia tunapenda kuvaa blauzi. Kwa mfano hapa nilipo nimevaa blauzi ambayo imeandikwa “*women of Africa*” yaani wanawake wa Afrika, kama ambavyo mtaona na picha zinawaonyesha hawa wanawake wa kiafrika jinsi wanavyonekana. Na nguo kama hizi mfano t-shirt kama hii ambayo nimeivaa, mara nyingi inatengenezwa kwa ajili ya kuwauzia watalii wanapoitembelea Tanzania. Kwa hiyo mara nyingi nguo kama hizi, blauzi kama hizi ambazo zina mambo ya kusifia ya Afrika, ya Tanzania, utakuta nyingi zipo katika maduka yale ambayo watalii wakija Tanzania wanapenda kutembelea na kwenda kununua vitu huko. Vilevile tuna vazi la kikoi, vazi hili, hii inaitwa ni kikoi, tunafunga kama ambavyo tunafunga khanga, kwa hiyo hiki ni kikoi lakini pia kimechorwa vizuri maua kama ambavyo mnaona, na yameandikwa “karibu Tanzania” “karibu Tanzania” kwa hiyo ni vazi ambalo wanawake wengi wa kitanzania wanapenda kuvaa. Na kama ambavyo nimesema, kwa mfano hapa kimeandikwa karibu Tanzania ni kwa ajili ya kuwahamasisha labda wageni au watalii ambao wanaitembelea Tanzania. Kwa hiyo utakuta mavazi kama haya pia yanapatikana katika maduka ambayo watalii wengi hupenda kwenda kutembelea na kununua nguo kule. Kwa hiyo katika tu maisha ya kawaida, watanzania tunavaa t-shirt, tunavaa hizi blauzi, pia tunavaa vikoi. Na vazi hili la vikoi limeingia sana katika kipindi cha hivi karibuni hasa katika miji mikubwa. Utakuta wanavaa vikoi wanawake na hata wanaume pia. Lakini asilimia kubwa ya wanaume ambao wanavaa vazi hili la kikoi, wapo katika mikoa ya pwani, yaani kule katika pwani utakuta wengi, tunawaita waswahili wa pwani, wengi wanapenda kuvaa vikoi. Kwa hiyo, karibuni Tanzania, kuna mavazi ya kila aina, haya ni baadhi tu ya mavazi ambayo nimeweza kuyazungumzia. Kwa hiyo kuna mavazi ya aina nyingi na ya aina mbalimbali ambayo watanzania tunajivunia kwamba tunayo, na ni mavazi ambayo ni mazuri na yanapendeza.

**English translation:**

Another kind of dress which I want to talk about is a blouse that many Tanzanians wear. As you can see right here, this is a blouse and written on it is “women of Africa.” It shows what these women of Africa look like. This kind of dress is made especially for tourists when they visit Tanzania. Most of the time dresses like this, which represent the good things of Africa or Tanzania, can be found in shops where tourists go and shop. Also, we have a style called *kikoi*, and we wear *kikoi* as we wear *kanga*. So this is a *kikoi* and it has been inscribed. It has “Welcome to Tanzania” written on it just to encourage tourists and visitors who visit Tanzania. *Kikoi* is a kind of dress which many women wear in everyday life. We also wear blouses. *Kikoi* dress has gained popularity in recent years, and is mostly worn by people in big cities. Both men and women wear *kikoi*, but a large percentage of men who wear *kikoi* can be found in coastal regions. We call these men *waswahili wa pwani*, which means “the Swahili men of the coast.” We have so many types of dresses. The ones I have talked about are just a few among many. So we Tanzanians are proud that we have a variety of nice dress styles and that they look good.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated